GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXVI Nam. 6675 **13 Novemba, 2017** **Bei Shs. 5,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti *Hutolewa kila Ijumaa*

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar Nam. 2 ya Mwaka 1995 na kutunga Sheria mpya ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji, Kuweka Masharti Bora zaidi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo 231

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili

Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar, Nam. 2 ya 1995 na kutunga Sheria Mpya

T A N G A Z O

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 6 Disemba, 2017 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
13 Novemba, 2017

(Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA
WA
SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA KUSIMAMIA MWENENDO WA BIASHARA NA KUMLINDA MTUMIAJI YA ZANZIBAR NAM. 2 YA MWAKA 1995 NA KUTUNGA SHERIA MPYA YA USHINDANI HALALI WA BIASHARA NA KUMLINDA MTUMIAJI, KUWEKA MASHARTI BORA ZAIDI PAMOJA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Ushindani halali wa Biashara na kumlinda mtumiaji ya Zanzibar, 2017 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais na kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Ufafanuzi.

2. Katika Sheria hii, isipokuwa pale ambapo itaelezwa vyenginevyo:

"kujipatia" kuhusiana na hisa au mali maana yake ni: upataji ama binafsi au wa pamoja na mtu mwengine, maslahi halali yoyote kisheria yatokanayo na hisa au mali, lakini haijumuishi upataji kwa njia ya kutoza tu;

"mahusiano"maana yake ni kuhusiana baina ya mtu mmoja na mwengine ikiwa rasmi au vyenginevyo, kwa uanahisa au kwa mambo mengine;

“makubaliano” maana yake ni makubaliano ya aina yoyote ikiwa yana nguvu kisheria au hayana baina ya mashirika yanayokusudiwa kufanya kazi ndani au sehemu yoyote ya Zanzibar, na yanajumuisha makubaliano ya mdomo, maamuzi ya jumuiya au kampuni na mashirikiano ya kibiashara;

“visaidizi vya kibiashara” maana yake ni huduma zote zinazotolewa, zikiwemo za kibenki, bima, usafiri, maghala, na matangazo yanayotumika kurahisisha biashara;

“kugawana wateja au masoko” maana yake ni kuweka makubaliano kwa njia ya maandishi au kimazingira ya kugawana masoko baina ya washindani kwa ajili ya kuziwekea mipaka haki za washindani katika kufanya biashara katika maeneo maalum yaliyotengwa, aina ya bidhaa iliyoanishwa, huduma, au wateja maalum walioanishwa, kwa lengo la kuondosha au kukwaza ushindani baina ya washindani hao;

"mienendo ya biashara isiyo ya ushindani" inajumuisha : shughuli kama vile upangaji wa bei, uhodhi wa soko, miungano, kufanya miungano, kugoma kwa pamoja kwa washindani, kuzuia bidhaa, kuuza bidhaa na kubana na mengine yanayohusiana na hayo;

“mali”, kwa madhumuni ya shirika, maana yake:

(a) mali halisi za shirika zinazoonekana, zikijumuisha hisa, dhamana nyengine za kifedha na alama za biashara;

(b) mali zote halisi za shirika zisizoonekana zikijumuisha mahusiano mazuri ya kibiashara, malibunifu na utaalamu;

"jumuia" maana yake ni kikundi ama kimejisajili kisheria au hakikusajiliwa, kinachoundwa ili kulinda na kuendeleza maslahi ya wanachama wake au watu wanaowakilishwa na wanachama wake;

“biashara” inajumuisha ufanyaji wa shughuli zote za kitaalamu au kazi zote zinazopelekea kupata malipo au zawadi;

“Mwenyekiti wa Tume” maana yake ni Mwenyekiti wa Tume ya Ushindani halali wa Biashara anaeteuliwa chini ya kifungu cha 7(1)(a);

“Mwenyekiti wa Baraza la Ushindani Halali” maana yake ni Mwenyekiti wa Baraza la Ushindani Halali wa Biashara anaeteuliwa chini ya kifungu cha 26(2) (a);

"kugoma kwa pamoja kwa washindani" maana yake:

(i) kuzuia upande mmoja kwenye makubaliano ya usambazaji wa bidhaa au huduma kwa watu fulani, au kupata bidhaa au huduma kutoka kwa watu fulani , walio katika ushindani na upande mwengine wa makubaliano; au

(ii) kuweka vikwazo au kudhibiti masharti na makubaliano au mazingira ambayo, kwa upande katika makubaliano hufanya usambazaji wa bidhaa au huduma kwa watu fulani, au kupata bidhaa au huduma kutoka kwa watu fulani katika ushindani na upande wowote kwenye makubaliano.

"kula njama katika kupata au kutoa zabuni" maana yake:

(i) kupanga au kudhibiti bei au masharti ya upataji au utoaji wa zabuni kwa washirika katika makubaliano kwenye mnada au upataji au utoaji wowote wa zabuni kwenye ushindani; au

(ii) kuzuia upande mmoja katika makubaliano katika kupata au kutoa zabuni kwenye mnada au katika kupata au kutoa zabuni ya aina yoyote kwenye ushindani.

"Tume" maana yake ni Tume ya Ushindani Halali wa Biashara Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4(1);

“kampuni” maana yake ni kampuni iliyosajiliwa kisheria iliyokuwa au isiyokuwa na ukomo wa dhima katika sehemu yoyote ya dunia au inayotambuliwa na sheria za Zanzibar;

"ushindani" maana yake ushindani katika soko ndani ya Zanzibar na unahusu mchakato ambapo watu wawili au zaidi:

(a) husambazwa au kudhamiria kusambazwa bidhaa au huduma ama zinazofanana au mbadala kwa watu walio katika soko moja kijiografia; au

(b) kupata au kudhamiria kupata bidhaa au huduma ama zinazofanana au mbadala kutoka kwa watu walio katika soko moja kijiografia;

“mshindani" maana yake ni mtu ambaye aliekatika ushindani na mtu mwengine, au angekuwa katika makubaliano ambayo watu wawili wanahusika na wanaweza kuwa katika ushindani baina yao;

“mienendo ya pamoja” maana yake ni mienendo inayojumuisha mawasiliano baina ya washindani ambao hawana makubaliano rasmi lakini hali hiyo haiathiri ushindani baina yao;

"mwenendo" unajumuisha kufanya au kukataa kufanya jambo lolote, kutofanya kwa makusudi jambo lolote, kubainisha kuwa jambo halitafanyika, kufanya makubaliano au kutekeleza makubaliano;

“mtumiaji” maana yake ni mtumiaji wa moja kwa moja au kwa namna nyengine wa bidhaa au huduma inayotolewa na shirika katika kufanya biashara, na inajumuisha:

(a) shirika linalotumia bidhaa hiyo au huduma hiyo iliyotolewa kama ni nyenzo katika biashara yake;

(b) muuzaji wa jumla, wa rejareja na mtumiaji wa mwisho;

(c) mtu yeyote ambaye huduma hiyo inatolewa kwake;

“mkataba wa mtumiaji” maana yake ni mkataba unaofungwa baina ya msambazaji wa huduma au bidhaa na mtumiaji wakati mkataba huo ni miongoni mwa:

(a) mkataba unaofuata sheria za Zanzibar au ambao unahusika na masharti Sehemu ya Saba ya Sheria hii; na

(b) ambapo, msingi wa mkataba huo ni bidhaa au huduma, bidhaa au huduma hizo ni za mtumiaji.

“mahakama” maana yake ni mahakama yenye mamlaka;

“ubandia wa bidhaa” maana yake:

(a) bila ya ruhusa ya mmiliki wa malibunifu ambaye ni mkaazi wa Zanzibar kwa bidhaa iliyodhibitiwa, utengenezaji, uzalishaji au ufanyaji, iwe Zanzibar au mahala pengine popote wa bidhaa zozote zilizodhibitiwa zimeigwa kwa namna na kiasi ambacho bidhaa hizo za wigo kwa kiwango kikubwa zimenakiliwa kutoka bidhaa zilizodhibitiwa;

(b) bila ya ruhusa ya mmiliki wa malibunifu ambaye ni mkaazi wa Zanzibar kwa bidhaa iliyodhibitiwa, utengenezaji, uzalishaji au ufanyaji, iwe Zanzibar au mahala pengine popote, kwa kuigwa kwa kitu chochote kinachuhusika na malibunifu kwa bidhaa hiyo kama rangi ambapo uigaji huo unamsababisha mtu kubabaika kwa kushindwa kujua uhalisia wa bidhaa hiyo au kudhani kwamba bidhaa hiyo ya wigo ni ile bidhaa halisi iliyodhibitiwa au iliyotengenezwa au kuzalishwa au kufanywa kwa ruhusa ya aliyeidhibiti;

“bidhaa bandia” maana yake ni bidhaa ambazo zinatokana na ufanyaji wa shughuli bandia na inajumuisha na njia zozote zile zinazotumika kwa madhumuni ya kughushi;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurungenzi Mkuu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 8(1);

“waraka” unajumuisha taarifa zilizonakiliwa kwa maandishi, zikiwa katika hali ya kieletroniki au katika mfumo mwengine wowote, pamoja na matumizi ya teknolojia yatakayowezesha taarifa hizo zilizopo katika hali ya kielektroniki kupatikana;

“ukiritimba wa soko” maana yake ni hali ambayo:

(a) mtu yeyote akiwa yeye peke yake,mtu huyo anaweza kuzuwia au kupunguza ushindani kwa kutumia faida au hali halisi katika soko hilo kwa muda;

(b) umiliki wa hisa katika soko wa mtu huyo ni zaidi ya asilimia 40;

“Shirika” maana yake mtu yeyote, taasisi ya kitaalamu, ubia, mashirika, kampuni, jumuia au mtu anaye tambulika kisheria ambaye anajihusisha na shughuli za biashara kwa ajili ya faida au tunzo, na inajumuisha matawi yake, shirika lake dogo,washirika wake au chombo chochote ambacho moja kwa moja au vyenginevyo kinadhibitiwa na shirika hilo;

"Matangazo ya uongo, upotoshaji au udanganyifu” maana yake ni matumizi ya kauli za uongo, upotoshaji au udanganyifu katika kutangaza na kwa kuhusiana na bidhaa kwa bidhaa zinazoingizwa

Zanzibar, inajumuisha matumizi ya lugha nyengine yoyote isiyokuwa Kiingereza au Kiswahili katika matangazo hayo na katika maandiko ya bidhaa hizo;

"bidhaa" maana yake ni aina zote za mali pamoja na mambo mengine, zinajumuisha:

(a) meli, ndege na magari;

(b) wanyama, wakiwemo samaki;

(c) madini, miti au mazao, vilivyopo juu, chini au vinavyoshikamana na ardhi au venginevyo;

(d) gesi au umeme;

(e) majengo na miundo mengine; na

(f) bidhaa za ndani au zilizoingizwa kutoka nje.

“Serikali” maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

“kundi" kuhusiana na shirika maana yake ni kampuni, au kampuni nyengine yoyote ambayo inamiliki kampuni au matawi yake na kampuni nyengine ambazo ni matawi ya kampuni zinazomilikiwa;

“makubaliano sawa” maana yake ni makubaliano baina ya mashirika ambayo, kwa madhumuni ya makubaliano hayo kuendesha shughuli za biashara katika soko la aina moja na lenye washindani wenye uwezo katika soko hilo;

"leseni" maana yake ni leseni, kibali au mamlaka yanayoruhusu mwenye leseni kufanya usambazaji ama kupata bidhaa au huduma au kufanya shughuli yoyote nyengine kibiashara;

"Soko" maana yake soko ndani ya Zanzibar, au sehemu ya Zanzibar na inakusudiwa uwezekano mbali mbali wa ubadilishanaji katika usambazaji au mahitaji baina ya aina makhsusi ya bidhaa au huduma na baina wasambazaji au wapataji au wasambazji mwenye uwezo au wapataji wa bidhaa hizo au huduma hizo;

"uzalishaji" maana yake ni ubadilishaji, kwa kiwango cha biashara wa malighafi kuwa bidhaa zilizokamilika au zisizo kamilika na inajumuisha ukusanyaji wa malighafi kwa bidhaa zilizokamilika au zisizo kamilika na haijumuishi shughuli za madini;

"vielelezo" vinajumuisha, taarifa yoyote, nyaraka au ushahidi;

“wajumbe wa Baraza la Ushindani Halali” maana yake ni mjumbe wa Baraza la Ushindani Halali walioainishwa chini ya kifungu cha 26(2) cha Sheria hii;

"miungano" maana yake ni upataji wa hisa,biashara, au mali nyingine iwe ndani au nje ya Zanzibar,unaopelekea mabadiliko ya umiliki wa biashara, sehemu ya biashara, au mali ya biashara ndani ya Zanzibar;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Biashara;

"kuzuwia uzalishaji baina ya washindani" maana yake ni washiriki katika makubaliano kuzuia, kuweka vikwazo au kudhibiti uzalishaji wa bidhaa au huduma zinazopaswa kusambazwa katika ushindani;

"mtu" maana yake ni mtu binadamu au chombo chochote kilichoanzishwa kisheria;

“eneo” linajumisha ardhi, jengo lolote, muundo, gari, meli, ndege au chombo cha kuhifadhia kitu;

“Rais” maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"kupanga bei baina ya washindani" maana yake ni kupanga, kuweka vikwazo, au kudhibiti bei, ushuru, malipo ya ziada au malipo mengine kwa ajili ya, au kwa makubaliano au masharti ambayo upande mmoja katika makubaliano husambaza au hupata; au huhiari kufanya usambazaji au kupata , bidhaa au huduma ,katika kushindana na upande wowote kwenye makubaliano;

“kuondoa bidhaa” maana yake ni kurejesha bidhaa kwa muuzaji au mzalishaji baada ya kugundua masuala ya usalama au kasoro kwenye bidhaa ambazo zinaweza kuhatarisha watumiaji au kumfanya mzalishaji au muuzaji kuwa katika hatari za kuchukuliwa hatua za kisheria;

“uchapishaji” unajumuisha uchapishaji kwa njia ya mtandao;

"kuuza" inajumuisha makubaliano yoyote ya kuuza au kutoa kwa ajili ya kuuza na inajumuisha kuzitoa bidhaa kwa ajili ya kuuza, kutoa nyaraka ya taarifa za bidhaa au huduma ikiwa kwa njia ya mdomo au maandishi, na kitendo chochote au taarifa ambayo inaeleza hiari ya kuingia kwenye muamala wa mauzo;

“Mrajis” maana yake ni mtu anayeteuliwa kuwa Mrajis wa Baraza la Ushindani Halali chini ya kifungu cha 28 (1) cha Sheria hii;

"huduma" inajumuisha kukubali au kutekeleza wajibu wowote ikiwa wajibu huo utazingatia ujuzi au vyenginevyo, kwa lengo la kupata au kuzawadiwa isipokuwa usambazaji wa bidhaa lakini haitojumuisha utoaji wa huduma chini ya mkataba wa ajira;

"Usambazaji" kuhusiana na:

(a) bidhaa maana yake ni kusambaza au kusambaza tena kwa njia ya kuuza, kubadilishana, kupangisha, kukodisha au kukodi kwa lengo la kununua; na

(b) huduma maana yake ni utoaji kwa njia ya kuuza, kutunuku au utoaji wa huduma;

"biashara" maana yake ni biashara ya kununua na kuuza bidhaa na inajumuisha shughuli zote za kibiashara;

"jumuiya ya biashara" maana yake ni mkusanyiko wa watu ulioanzishwa kwa madhumuni ya kuendeleza maslahi ya kibiashara kwa wanachama wake au watu wanaowakilishwa na wanachama wake;

"mienendo ya kibiashara" maana yake mienendo yote inayohusiana na biashara na biashara yoyote na inajumuisha kitu chochote kile kilichofanywa au kimependekezwa kufanywa na mtu yeyote ambacho kinaathiri au kinaweza kuathiri utaratibu wa ufanyaji biashara kwa mfanya biashara yeyote au tabaka la wafanyabiashara au uzalishaji, usambazaji, au bei katika utekelezaji wa shughuli za biashara kwa bidhaa yoyote, ikiwa halisi au ya mtu binafsi au ya huduma yoyote;

"Baraza" maana yake ni Baraza la Ushindani halali wa Biashara linaloanzishwa chini ya kifungu cha 26 (1);

"Nishati" maana yake ni umeme, usambazji wa maji safi na maji taka, petroli, na mambo mengine yatakayo tambuliwa na Waziri;

" ZURA" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar;

"ZMA" maana yake ni Mamlaka ya Usafiri Baharini;

"ZFDA" maana yake Wakala wa kusimamia Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar;

"ZBS" maana yake ni Taasisi ya Viwango Zanzibar.

Matumizi ya Sheria hii.

3.-(1) Sheria hii itatumika kwa taasisi au mashirika ya kibiashara, vyombo vya Serikali, na Serikali za Mitaa zinazohusika na ushindani na kumlinda mtumiaji.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, bila ya kuathiri maana katika hali nyengine, neno "biashara" maana yake ni kuuza au kupata shughuli ya biashara, sehemu ya shughuli ya biashara au rasilimali ya biashara inayofanywa na kampuni au Shirika, chombo cha Serikali au Serikali za Mitaa zinazojihusisha katika biashara; na

(3) Yafuatayo hayamaanishi na kujihusisha katika biashara:

(a) utozaji au ukusanyaji wa kodi;

(b) utoaji au ubatilishaji wa leseni, vibali na dhamana;

(c) ukusanyaji wa ada za leseni, vibali na dhamana;

(d) miamala ya ndani ya Serikali, chombo cha Serikali au Serikali za Mitaa.

(4) Matumizi yote ya Sheria hii katika kusambaza:

(a) bidhaa, yatajulikana kama usambazaji wa bidhaa ndani au kutoka Zanzibar;

(b) huduma, yatajulikana kama usambazaji wa huduma ndani au kutoka Zanzibar.

SEHEMU YA PILI
TUME YA USHINDANI HALALI WA BIASHARA

Uanzishwaji wa Tume.

4.-(1) Kunaanzishwa Tume itakayojulikana kama Tume ya Ushindani halali wa Biashara kutekeleza kazi kwa mujibu wa mipaka, uwezo na mamlaka iliyopewa kisheria au chini ya Sheria hii.

(2) Tume itakuwa ni chombo cha Serikali chenye uwezo wa kurithi au kurithiwa na itakuwa na muhuri wake, Kwa kutumia jina lake, Tume itakuwa na uwezo wa:

(a) kushitaki na kushitakiwa;

(b) kuchukuwa, kununua, kuhodhi au vyenginevyo kujipatia, kuzuia, kutoza au kuondosha mali inayohamishika na mali isiyohamishika;

(c) kuingia mikataba; na

(d) kufanya au kutekeleza mambo mengine yote au vitu kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake chini ya Sheria hii

ambayo yanaweza kisheria kufanywa au kutekelezwa na chombo kinachojitegemea.

Kazi za Tume.

5.-(1) Kazi za Tume zitakuwa ni:

(a) kusimamia, kudhibiti na kuzuia matendo yoyote yanayoathiri ushindani na uendeshaji wa biashara halali Zanzibar;

(b) kufanya uchunguzi juu ya tuhuma yoyote ikiwa imeanzisha yenyewe au baada ya kupokea malalamiko ya mtu kwa lengo la kuendesha biashara ili kutambua kama mtu au Shirika limefanya biashara isiyokuwa ya ushindani Halali;

(c) kusimamia bei za bidhaa zinazodhibitiwa na kupanga bei elekezi kwa bidhaa hizo;

(d) kufanya utafiti na Kukusanya taarifa zinazohusiana na gharama, usambazaji wa bidhaa zinazodhibitiwa na zisidhozibitiwa na kutoa mapendekezo yanayofaa;

(e) kufanya uchunguzi kwa matakwa ya Tume yenyewe au kwa maombi ya mtu ambaye ameathiriwa na miungano ya makampuni iliyotokea;

(f) kuchukua hatua au njia muhimu ambazo zitalinda au kuondosha uwepo wa miungano ya makampuni isiyofaa au matumizi mabaya ya kuhodhi soko;

(g) kutoa taarifa kwa mtu yeyote anayejihusisha na biashara kwa kuzingatia haki na wajibu kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(h) kutoa taarifa na miongozo kwa watumiaji kwa kuzingatia haki na wajibu chini ya Sheria hii;

(i) kufanya utafiti na kutoa taarifa kwa umma unaohusiana na utekelezaji wa masharti ya Sheria hii na kusambazwa kwa jamii;

(j) kusikiliza mashauri ya mtu mmoja mmoja au kikundi cha watu wenye maslahi yanayohusiana na utekelezaji wa Sheria hii;

(k) kuhakikisha iwapo mienendo ya biashara iliyokatazwa inafanyika au imefanyika;

(l) kusimamia ipasavyo uendeshaji na ufanyaji kazi wa Tume kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(m) kushajihisha na kusimamia utekelezaji wa Sheria hii;

(n) kukuza uelewa wa jamii juu ya kufahamu wajibu, haki na fidia chini ya Sheria hii na wajibu, majukumu, na shughuli za Tume;

(o) kuwezesha upatikanaji wa taarifa na miongozo kwa watumiaji inayohusiana na wajibu wa watu chini ya Sheria hii na haki na fidia zinazopatikana kwa watumiaji chini ya Sheria hii;

(p) kufanya uchunguzi, na utafiti kwenye mambo yanayohusu ushindani na kulinda maslahi ya watumiaji;

(q) kufanya uchunguzi ili kuondoa vikwazo katika ushindani vinavyohusiana na kuingia na kutoka katika soko na uchumi kwa ujumla kwa sekta husika na kutoa matokeo ya athari hizo;

(r) kufanya utafiti unaohusiana na sera, taratibu na mipango ya mamlaka za udhibiti ili kuhakiki athari zake kwenye ushindani na ustawi wa mtumiaji na kutangaza matokeo ya utafiti huo;

(s) kushauriana na jumuiya za watumiaji, mamlaka za udhibiti, asasi za kibiashara na watu wengine wenye maslahi yanayofungamana na masuala ya ufanyaji wa biashara halali na ushindani;

(t) kufanya mambo yote muhimu yanayohusiana na utekelezaji mzuri wa kazi zake kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Uwezo ya Tume.

6. Tume itakuwa na uwezo ufuatao:

(a) kutoa amri na maelekezo kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(b) kutoza adhabu za kifedha au fidia kwa shirika lolote ambalo linaendesha biashara kinyume na masharti ya Sheria hii;

(c) kulitaka shirika lolote la kibiashara kutoa taarifa kwa Tume itakapohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake;

(d) kufanya uchunguzi juu ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii;

(e) kuingia sehemu yoyote na kufanya ukaguzi baada ya kuidhinishwa na Tume;

(f) kuchunguza nyaraka au vivuli vya nyaraka au sehemu ya nyaraka na kuvizuiya pale ambapo itakapoona inafaa;

(g) kuteua mtaalamu ambaye atasaidia kufanya utafiti na uchunguzi katika maeneo ambayo yamo chini ya mamlaka ya Sheria hii;

(h) kuchukua sampuli za bidhaa kwa ajili ya kufanya uchunguzi;

(i) kuweka tozo au malipo yaliyokubaliwa kama yatakavyoainishwa chini ya Sheria au kanuni za Sheria hii;

(j) kuzuia bidhaa bandia na zisizofaa ambazo hazikufikia kiwango na kuziharibu kwa kushirikiana na mamlaka nyengine.

Wajumbe wa Tume.

7.-(1) Tume itaundwa na Wajumbe sita kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais na ambaye atalazimika kuwa na angalau shahada ya kwanza katika fani ya Uchumi, Uongozi wa Biashara, Utawala wa Umma, Fedha au Sheria pamoja na uzoefu wa angalau miaka kumi;

(b) Mkurugenzi Mkuu ambaye atakayeingia kwa nafasi yake; na

(c) Wajumbe wengine wanne watakaoteuliwa na Waziri.

(2) Wajumbe wengine wa Tume watakuwa na sifa ya kuteuliwa na Waziri ikiwa wana taaluma na uzoefu katika masuala ya viwanda, biashara, uchumi, sheria, utawala wa umma au fani zinazolingana na hizo.

(3) Katika Kuteua wajumbe chini ya kifungu kidogo cha (1) (c) Waziri atazingatia ushiriki wa Sekta Binafsi.

Sekretarieti ya Tume.

8.-(1) Kunaanzishwa Sekretarieti ya Tume ambayo itakayoongozwa na Mkurugenzi Mkuu ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya Uongozi wa Biashara, Uchumi, Usimamizi wa Biashara, Sheria, Utawala wa Umma au fani inayolingana kutoka Chuo Kikuu kinachotambulika;

(c) ana uzoefu wa kazi angalau wa miaka kumi katika fani zilizoainishwa chini ya kifungu hiki.

Kazi za Sekretarieti.

9. Sekretarieti itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Tume;

(b) kutekeleza kazi za kila siku za Tume na maamuzi yote yaliyofanywa na Tume;

(c) kutayarisha taarifa ya utekelezaji ya kila mwaka na kuiwasilisha kwa Tume;

(d) kutayarisha bajeti na kalenda ya utekelezaji wa kazi za Tume;

(e) kuandaa na kutekeleza kwa ufanisi mpango mkakati; na

(f) kufanya kazi nyengine yoyote kama itakavyoelekezwa na Tume.

Muda wa utumishi wa Wajumbe.

10. Mwenyekiti na wajumbe wengine wanne wa Tume watatumikia ofisi kwa muda maalum uliowekwa kama ifuatavyo na wataweza kuteuliwa tena:

(a) Mwenyekiti miaka minne;

(b) Wajumbe wengine wanne miaka mitatu.

Maposho.

11. Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Tume watastahiki kulipwa posho na maslahi mengine kama Waziri atakavyoamua kipindi baada ya kipindi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Ukomo wa Ujumbe.

12. Nafasi ya mjumbe itakuwa wazi:

(a) akifariki;

(b) ikiwa, bila ya dharura ya msingi, atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Tume;

(c) ikiwa atajiuzulu au atakua kwa namna yoyote amekosa sifa ya kuwa mjumbe wa Tume; au

(d)ikiwa ameshindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu za kimwili au kiakili.

Vikao vya Tume.

13.-(1) Tume itakutana kawaida mara moja kila miezi mitatu na inaweza kukutana wakati wowote ikihitajika kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake.

(2) Mkurugenzi Mkuu ataitisha vikao vya Tume kama atakavyoagizwa na Mwenyekiti.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) na (2) vya kifungu hiki Mwenyekiti anaweza kuitisha kikao, baada ya kushauriana na wajumbe, wakati na mahali ambapo panatambulika na Serikali.

(4) Mwenyekiti ataendesha vikao vya Tume na iwapo Mwenyekiti hayupo, wajumbe wanaweza kumteua Makamo Mwenyekiti kutoka miongoni mwao kuendesha vikao.

(5) Akidi itakuwa ni wajumbe watatu ikijumuisha Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti.

(6) Mambo yote yataamuliwa kwa kura nyingi za wajumbe waliohudhuria, itakapotokea kura kuwa sawa, mjumbe anayeendesha kikao atakua na kura ya maamuzi.

(7) Mwenyekiti anaweza kuamua kwamba baadhi ya vikao vya Tume vifanyike kwa simu, kwa televisheni au kwa njia yoyote ile ya mawasiliano ambapo mwenyekiti ataona inafaa.

(8) kumbukumbu za maazimio zitasainiwa na wajumbe wote wa Tume na zitatambulika kwamba ni maazimio halali ya tume ikiwa maazimio hayo yatapitishwa katika mkutano halali wa Tume.

Kukasimisha Madaraka.

14. Tume inaweza kukasimu madaraka kwa Uongozi kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Kuanzisha lalamiko.

15.-(1) Tume chini ya utaratibu iliyojipangia inaweza ikachukua hatua za kisheria dhidi ya makosa ya taratibu za kibiashara zilizokatazwa.

(2) Mtu yeyote anaweza:

(a) kuwasilisha taarifa kuhusu uwepo wa vitendo vya kibiashara vilivyokatazwa kwa Tume, katika utaratibu wowote unaofaa, au

(b) kuwasilisha malalamiko dhidi ya vitendo vya kibiashara vilivyokatazwa kwa Tume.

(3) Tume itazingatia malalamiko ya Mtumiaji na kutoa maamuzi dhidi ya malalamiko hayo.

(4) Endapo mtu yeyote au mlalamikaji ambaye hakuridhika na maamuzi yaliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki anaweza kukata rufaa kwa Baraza la Ushindani.

Jumuia za watumiaji.

16.-(1) Watumiaji wanaweza kuanzisha jumuia zao wenyewe kutengeneza jukwaa kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali ya kumlinda Mtumiaji na kuyapeleka tume kwa kuzingatiwa.

(2) Watumiaji wanaweza kushauriana na Tume juu ya masuala yote ya biashara yanayohusiana na ushindani Halali na kumlinda Mtumiaji.

Uanzishwaji wa vitengo vya Tume.

17.-(1) Tume itaanzisha kitengo kimoja au zaidi katika kutekeleza kazi zake kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(2) Vitengo vilivyoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki vitajumuisha vitengo vitakavyohusiana na:

(a) mienendo ya biashara inayokatazwa;

(b) kumlinda Mtumiaji na udhibiti wa bidhaa bandia;

(c) uendeshaji wa Tume; na

(d) kitengo chochote ambacho Tume itaona inafaa kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

Wafanyakazi wa Tume.

18.-(l) Tume itaajiri wafanyakazi wanaofaa ili kuiwezesha kumudu kazi na utekelezaji wa mamlaka yake kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Tume inaweza kutafuta Mshauri mwelekezi au mtaalamu ambaye anaonekana ni sahihi kuisaidia kutekeleza kazi na mamlaka yake kama yalivyoainishwa na Sheria hii.

Usiri.

19.-(1) Mtu yeyote anayetoa au kufichua jambo lolote kwa Tume, ama kwa kulazimika kisheria au vyenginevyo, anaweza kudai kwa taarifa aliyotoa iwe siri kuhusiana na jambo hilo au sehemu yake yoyote.

(2) Madai ya siri yanaweza kutolewa muda wowote kabla jambo halijafichuliwa kwa watu walio nje ya Tume bila ya kukiuka masharti ya kifungu hiki.

(3) Iwapo ushahidi utatolewa kwa mdomo, madai yanaweza kufanywa kwa mdomo wakati wa kutoa ushahidi, na katika hali nyengine zozote ni lazima madai yawe kwa maandishi kusainiwa na mtu anaetoa madai hayo na kuainisha vielezo vyote yanayohusika na kueleza sababu ya madai.

(4) Iwapo Tume imeridhika kwamba vielelezo hivyo ni vya siri na :

(a) kuviweka bayana kunaweza kuathiri vibaya nafasi ya ushindani ya mtu yeyote; au

(b) ni nyeti kibiashara kwa sababu fulani,

Tume itaviweka vielelezo hivyo katika hali ya usiri.

(5) Mtu ambaye atakiuka masharti ya kifungu hiki, amefanya kosa na itakapothibitika atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja na isiyozidi Shilingi Milioni Tano au kifungo kwa muda usiopungua miezi sita na usiozidi miaka miwili au vyote viwili faini na kifungo.

Mgongano wa maslahi.

20.-(1) Mfanyakazi au Wajumbe au mfanyakazi wa Tume atachukuliwa kuwa ana mgongano wa kimaslahi kwa mujibu wa Sheria hii ikiwa atapata maslahi ya kifedha, maslahi kutokana na mahusiano binafs au maslahi mengine yoyote ambayo yanaweza kuleta mgongano katika utekelezaji mzuri wa kazi.

(2) Ikiwa katika muda wowote mfanyakazi au wajumbe au mfanyakazi wa Tume atakuwa na mgongano wa kimaslahi kuhusiana na:

(a) jambo lolote liliopo mbele ya Tume kwa kusikilizwa au kuamuliwa; au

(b) jambo lolote ambalo Tume inaweza kutarajia kuletwa mbele yake kwa kusikilizwa au kutolewa uamuzi,

ataeleza mara moja mgongano wa kimaslahi kwa wajumbe wengine wa Tume na kuacha kushiriki, au kuendelea kushiriki katika jambo lolote la kufikiria au kutolea uamuzi.

(3) Pale ambapo tume itafahamu kwamba mfanyakazi au mjumbe ana mgongano wa kimaslahi kuhusiana na jambo lolote mbele ya Tume, Tume itamtaka mfanyakazi au mjumbe kuacha kushiriki au kushiriki kwa namna yoyote katika kushughulikia au kulitolea uamuzi jambo hilo.

Fedha za Tume.

21.-(1)Fedha za Tume zitajumuisha :

(a) fedha inayoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) fedha inayotolewa kwa Tume kutoka fedha za ZURA, ZMA na mamlaka nyingine za udhibiti kwa kazi zinazofanywa na Tume au zilizoelezwa kwenye sheria nyingine husika au kama itakavyoafikiwa kati ya Tume na mamlaka hizo;

(c) misaada yoyote, michango, na michango mingine inayotolewa kwa Tume.

(d) ada inayokusanywa na Tume; na

(e) malipo mengine yoyote ambayo ni stahili ya Tume kutokana na jambo lolote linalohusu shughuli za Tume.

Matumizi ya fedha za Tume.

22. Fedha za Tume zitatumika kwa ajili ya kuendesha shughuli za Tume.

Hesabu na ukaguzi wa Fedha.

23.-(1) Tume itatunza vitabu vya hesabu na kutunza kumbukumbu kwa muda usiozidi miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha na itatayarisha taarifa zifuatazo:

(a) Taarifa za mali na madeni ya Tume katika kipindi cha mwisho wa mwaka wa fedha, kuziwasilisha na kukaguliwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali.

(b) Taarifa za mapato na matumizi kwa kipindi cha mwaka huo wa fedha.

(c) Ripoti yoyote ya fedha kama itakavyo hitajika.

(2) Mapato yote yaliyokusanywa kwa huduma zilizotolewa na Tume yatawekwa Benki kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Ripoti ya mwaka.

24. Sekretarieti ya Tume ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha na baada ya kuthibitishwa na Tume, itawasilisha kwa Waziri Ripoti ya mwaka kwa mwaka husika ikijumuisha mambo yafuatayo:

(a) nakala za hesabu za Tume zilizokaguliwa, pamoja na ripoti ya ukaguzi.

(b) ripoti ya utekelezaji wa malengo na taarifa zinazohusiana nazo.

(c) ripoti ya utekelezaji ya kazi za Tume kwa kupindi cha mwaka wa fedha ; na

(d) taarifa nyengine za shughuli za Tume kama zitavyohitajika na Waziri.

Bajeti.

25. Kabla ya Mwisho wa kila mwaka wa fedha,Tume itaandaa au kupelekea kuandaliwa kwa bajeti kuhusu mwaka wa fedha unaofuata ikionesha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka huo wa fedha na itawasilisha bajeti hiyo kwa Waziri.

SEHEMU YA TATU
BARAZA LA USHINDANI HALALI

Baraza la Ushindani halali.

26.-(1) Kunaanzishwa Baraza litakalojulikana kama Baraza la Ushindani Halali wa Biashara kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yaliyoainishwa chini ya sheria hii.

(2) Baraza litaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Jaji Mkuu;

(b) wajumbe wengine wanne ambao watateuliwa na Waziri.

(3) Mwenyekiti alieainishwa chini ya kifungu kidogo cha (2) (a) cha kifungu hiki atakuwa Jaji wa Mahakama Kuu.

(4) Katika uteuzi wa wajumbe chini ya kifungu kidogo (2) (b) cha kifungu hiki, Waziri atateua watu wenye elimu na uzoefu katika fani yaSheria, Uchumi, Biashara, Fedha na fani nyengine zinazohusiana na hizo kutoka sekta ya umma na binafsi.

(5) Wajumbe wa Baraza watatumikia ofisi kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena.

(6) Akidi ya kuendesha vikao vya Baraza itakuwa ni Mwenyeketi wa Baraza na wajumbe wengine wawili.

Mjumbe mwalikwa.

27. Baraza katika kutekeleza kazi zake linaweza kumualika mtu yeyote kushiriki katika kufanikisha maamuzi ya Baraza.

Mrajisi wa Baraza.

28.-(1) Waziri atateua Mwanasheria kuwa Mrajis wa Baraza.

(2) Mrajisi atafanya kazi zote za utawala za Baraza kama zilivyoainishwa chini ya Sheria hii na kanuni zake.

(3) Mrajisi baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa Baraza ataitisha vikao vya wajumbe kujadili masuala au mambo yaliyowasilishwa kwa Baraza.

Kanuni za maadili.

29.-(1) Baraza litaweka kanuni za maadili zinazoweka viwango vya tabia vitakavyozingatiwa kwa wajumbe na waajiriwa wa Baraza katika utekelezaji wa majukumu yao.

(2) Kanuni za maadili zilizowekwa au kulezwa katika kifungu hiki zitakuwa na nguvu za kisheria kwa Baraza, wajumbe na waajiriwa wake.

Muhuri wa Baraza.

30.-(1) Baraza litakuwa na muhuri ambao utakuwa chini ya ofisi ya Mrajis.

(2) Muhuri wa Baraza kwenye waraka wowote utathibitishwa kwa kutiwa saini ya Mwenyekiti au Mrajis wa Baraza.

Kuondolewa ofisini mjumbe.

31. Waziri anaweza kumuondoa mjumbe katika ofisi, wakati wowote mjumbe huyo atakapokuwa na mambo yafuatayo:

(a) atakapojivunjia heshima mwenyewe;

(b) atakapo kuwa hana uwezo wa kufanya kazi zake kwa kuwa mgonjwa, au kuwa na matatizo ya kiafya au ya kiakili;

(c) amevunja masharti ya Sheria hii au kanuni za maadili ambazo Baraza linatakiwa kuzifuata;

(d) kushindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Baraza bila kutoa taarifa;

(e) kupata fedha au maslahi mengine ambayo yanaweza kuathiri kazi za Baraza;

(f) kutumia vibaya nafasi yake ambayo itapelekea kuathiri maslahi ya umma; au

(g) ikiwa atajiuzulu nafasi yake.

(2) Waziri atalazimika kumuondoa mtu kuwa mjumbe wa Baraza baada ya kufanya uchunguzi.

Kazi za Baraza.

32.-(1) Baraza litakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kusikiliza na kuamua rufaa zilizofanyiwa maamuzi na Tume ya ushindani Halali wa Biashara na mamlaka nyengine za udhibiti;

(b) kutoa waranti;

(c) kutoa maamuzi ya mashauri;

(d) kuweka kumbukumbu za rufaa na maamuzi ya Baraza na kupeleka kwa Mrajis;

(e) kuteleleza kazi na uwezo mwengine ulioainishwa katika Sheria hii;

(2) Baraza litatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii, na kuongozwa na misingi ya utawala wa Sheria.

Uwezo wa Baraza.

33.-(1) Baraza katika kutekeleza kazi zake litakuwa na mamlaka yafuatayo:

(a) kuhakikisha uwepo wa mashahidi na kuwasikiliza kwa kuwalisha kiapo au vyenginevyo;

(b) kulazimisha upatikanaji wa nyaraka; na

(c) kuihoji Tume au kutaka kuwasikiliza mashahidi hata walioko nje ya Nchi.

(2) Baraza litakamilika wakati wowote ikiwa mwenyekiti na wajumbe wawili watakuwepo.

(3) Maamuzi yoyote yatahesabika kuwa maamuzi ya Baraza ikiwa yatapitishwa na wajumbe walio wengi.

(4) Shahidi mbele ya Baraza atakuwa na kinga na fursa kama ilivyo katika Mahakama Kuu.

Maamuzi na amri za Baraza.

34.-(1) Maamuzi na amri za Baraza zitatolewa na kutekelezwa sawa sawa kama maamuzi na amri za Mahakama Kuu.

(2) Maamuzi na amri za Baraza katika jambo lolote kama ilivyolekezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, zinaweza kukatiwa rufaa Mahakama ya Rufaa na upande ulioathirika.

Mishahara na maposho.

35. Wajumbe na Mrajis wa Baraza watalipwa mishahara na maposho yao kama vile Waziri atakavyopanga kila baada ya muda kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma.

Pingamizi kwa Baraza.

36.-(1) Mtu yeyote ambaye:

(a) ataitwa mbele ya Baraza na akishindwa au kukataa kufika bila ya sababu za msingi;

(b) atafika kama shahidi, akakataa au kushindwa kula kiapo au kufanya uthibitisho kama alivyotakiwa na Baraza;

(c) atatoa maelezo yoyote mbele ya Baraza huku akijua kuwa ni ya uongo au wakati hana sababu za kuamini kuwa ni ya ukweli;

(d) ataacha kutoa au ataficha taarifa yoyote iliyotakiwa na Baraza katika kutekeleza kazi zake au inayohusu utekelezaji wa kazi hizo; au

(e) kwa namna yoyote inayopotosha, atazuia, atafedhehesha au kusumbua Baraza,

atakuwa ametenda kosa na atawajibika kulipa faini isiyopungua laki tano na isiyozidi milioni moja au kifungo kwa muda usiopungua miezi mitatu na usiozidi mwaka mwaka mmoja au vyote viwili faini na kifungo.

Kanuni za Baraza.

37. Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, na itakapo thibitishwa na Waziri, Baraza litatunga kanuni:

(a) kueleza namna rufaa itakavyowasilishwa kwenye Baraza na kiwango cha ada kuhusiana na rufaa;

(b) kueleza taratibu za Baraza katika kusikiliza rufaa na namna ya kutunza kumbukumbu za Baraza;

(c) kueleza namna ya kuitisha vikao vya Baraza, mahali na muda ambao vikao vitafanyika;

(d) kwa minajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii. kuhusiana na Baraza pamoja na rufaa kwa Baraza.

Fedha za Baraza.

38.-(1) Fedha za Baraza zitajumuisha:

(a) fedha inayoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) fedha inayotolewa kwa Baraza kutoka fedha za ZURA, ZMA na mamlaka nyingine zilizoelezwa kwenye sheria nyingine husika au kama itakavyoafikiwa kati ya Baraza na mamlaka hizo;

(c) misaada yoyote, michango, na michango mingine inayotolewa kwa Baraza;

(d) ada inayokusanywa na Baraza ; na

(e) malipo mengine yoyote ambayo ni stahili ya Baraza kutokana na jambo lolote linalohusu shughuli za Baraza.

Matumizi ya fedha za Baraza.

39. Fedha za Baraza zitatumika kwa ajili ya kuendesha shughuli za Baraza.

Hesabu na ukaguzi wa fedha.

40. Baraza litatunza vitabu vya hesabu na kutunza kumbukumbu kwa muda usiozidi miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha na itatayarisha taarifa zifuatazo:

(a) taarifa za mali na madeni ya Baraza katika kipindi cha mwisho wa mwaka wa fedha, kuziwasilisha na kukaguliwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali;

(b) taarifa za mapato na matumizi kwa kipindi cha mwaka huo wa fedha;

(c) ripoti yoyote ya fedha kama itakavyo hitajika.

(2) Mapato yote yaliyokusanywa kwa huduma zilizotolewa na Baraza yatawekwa Benki kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Ripoti ya mwaka.

41. Mrajisi wa Baraza ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha na baada ya kuthibitishwa na Baraza, atawasilisha kwa Waziri Ripoti ya Mwaka husika ikijumuisha mambo yafuatayo:

(a) nakala za hesabu za Baraza zilizokaguliwa, pamoja na ripoti ya ukaguzi;

(b) ripoti ya utekelezaji wa malengo na taarifa zinazohusiana nazo;

(c) ripoti ya utekelezaji ya kazi za Baraza kwa kupindi cha mwaka wa fedha; na

(d) taarifa nyengine za shughuli za Baraza kama zitavyohitajika na Waziri.

Bajeti.

42. Kabla ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, Baraza litaandaa au kupelekea kuandaliwa bajeti kuhusu mwaka wa fedha unaofuata ikionesha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka huo wa fedha na litawasilisha bajeti hiyo kwa Waziri.

SEHEMU YA NNE
MIENENDO YA BIASHARA INAYOKATAZWA

Mienendo ya biashara isiyo ya Ushindani.

43.- (1) Makubaliano, maamuzi au mienendo yoyote yenye madhumuni ya kuzuwia, kukwaza au kuvuruga ushindani yatajulikana moja kwa moja kama mienendo ya biashara isiyo ya ushindani, na kwa kifungu hiki yanakatazwa.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, shirika litajiepusha na mienendo ifuatayo ambayo inaharibu au inatengeneza ukiritimba katika nguvu za soko:

(a) kutumia utaratibu wa kupanga bei ili kuwaengua washindani;

(b) kuweka ubaguzi wa bei, katika usambazaji, au ununuzi wa bidhaa au huduma;

(c) kuweka vikwazo na masharti katika uzalishaji, usambazaji au ununuzi wa bidhaa au huduma;

(d) miungano, uchukuaji, ubia, au ununuzi kwa lengo la kudhibiti soko; au

(e) kuunganisha wazalishaji wawili au zaidi, wauzaji wa jumla, wauzaji wa reja reja, wahandisi, au wasambazaji wa huduma, katika kupanga bei ya aina moja ili kuengua ushindani.

(3) Mtu anaekiuka masharti ya kifungu hiki ametenda kosa.

Mikataba ya biashara isiyo ya Ushindani.

44.-(1) Mtu hataruhusiwa kufanya au kutekeleza makubaliano yenye madhumuni ya kuzuwia, kukwaza au kuvuruga ushindani.

(2) Makubaliano yoyote yatakayo kwenda kinyume na kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hayatoweza kutekelezwa chini ya Sheria hii.

(3) Kifungu hiki hakihusiki na makubaliano yenye lengo la miungano ya kibiashara ambayo hayana lengo la kuhodhi soko.

(4) Mtu anaekiuka masharti ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja na isiyozidi Shilingi Milioni Tano, au kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita au vyote viwili faini na kifungu.

(5) Mtu yeyote ambaye ameathirika na makubaliano ya biashara yasiyo ya ushindani au mienendo ya biashara anaweza kupeleka malalamiko yake kwa Tume kwa ajili ya fidia na Mkurugenzi Mkuu anaweza, kwa niaba ya Tume ikiwa ataridhika kwa mujibu wa mazingira ya yanayohusiana na shauri hilo, atawaamrisha wahusika waliohusika na makubaliano hayo yasiyo ya ushindani kumlipa muathirika fidia kama Tume itakavyoona inafaa.

Kukatazwa kwa baadhi ya makubaliano bila ya kujali athari zake katika ushindani.

45.-(1) Ni marufuku kwa mtu kufanya au kutekeleza makubaliano yoyote iwapo makubaliano hayo ni;

(a) kupanga bei baina ya washindani;

(b) kususa kwa pamoja kwa washindani;

(c) kupunguza uzalishaji baina ya washindani;

(d) kula njama katika kupata au kutoa zabuni; au

(e) kugawana wateja au masoko kwa madhumuni yoyote yasiyo ya ushindani.

(2) Makubaliano yanayoenda kinyume na masharti ya kifungu hiki hayatoweza kutekelezwa chini ya Sheria hii.

(3) Mtu yoyote anaekwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki ametenda kosa.

Kuzuia na kukataza kusambaza bidhaa.

46. Ni marufuku kwa mtu yeyote iwe yeye mwenyewe binafsi, kupitia wakala wake au shirika lolote au kwa kushirikiana na jengine au kupitia utaratibu au makubaliano yoyote:

(a) kuzuia bidhaa ili kuzifanya ziwe adimu iwe kwa madhumuni ya kufanya bei ipande au la;

(b) kuzuia huko kwa bidhaa kwa madhumuni ya kupandisha bei;

(c) kuharibu bidhaa au kuzipa ugumu wa kupatikana au kuharibu njia za uzalishaji na usambazaji iwe moja kwa moja au vyenginenyo kwa lengo la kuleta upungufu wa bidhaa hiyo au kupandisha bei.

Makubaliano ya biashara.

47.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hiimakubaliano ya biashara yafuatayo yanakatazwa:

(a) kuweka bei baina ya watu wanaojishughulisha na biashara ya bidhaa au huduma;

(b) kuzuia au kuweka masharti kwa kuuza au kusambaza au kununua au kwa bidhaa zilizonunuliwa au huduma;

(c) kula njama katika kupata au kutoa zabuni kwa lengo la kuzuia ushindani;

(d) kufanya vitendo vyovyote kwa pamoja kwa lengo la kulazimisha kufanyika makubaliano yatakayopelekea kuathiri ushindani;

(e) kukataa kusambaza bidhaa au huduma kwa wanunuzi au watumiaji; au

(f) kukataa moja kwa moja au vyenginevyo kuruhusu utaratibu au umoja wowote ambao unahitajika na ni muhimu katika ushindani.

(2) Mtu anaekiuka masharti ya kifungu hiki ametenda kosa.

Matumizi mabaya ya nguvu za soko.

48.- (1) Ni marufuku kwa mtu mwenye ukiritimba wa soko kutumia nafasi yake kwa madhumuni ya kuzuwia, kukwaza au kuvuruga ushindani.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki , ni marufuku kwa mtu mwenye ukiritimba katika soko husika:

(a) kutoza moja kwa moja au kwa namna nyengine bei ya juu au ya chini ya kuuzia au ya kununua au kuweka masharti ya biashara yaliyokuwa si halali;

(b) kuzuia uzalishaji, maendeleo ya kiufundi na ubunifu kwa ajili ya kumkandamiza mtumiaji;

(c) kufanya ubaguzi baina ya watumiaji au wasambazaji au;

(d) kufanya vitendo vyengine vyovyote vinavyofanana na hivyo ambavyo ni matumizi mabaya ya nguvu za soko.

(3) Ni marufuku kwa mtu mwenye ukiritimba katika soko kujihusisha katika mienendo inayowaondoa au inayokusudia kuwaondoa washindani katika soko kwa kufanya:

(a) bei lazimishi;

(b) kukandamiza bei;

(c) mtambuko wa ruzuku;

(d) kugawana soko; au

(e) mienendo mengine yoyote inayofanana na hiyo.

(4) Ni marufuku kwa mtu mwenye ukiritimba katika soko husika kujihusisha na mienendo yoyote ambayo itaathiri nafasi ya ushindani kwa washindani, kwa:

(a) kukataa kushirikiana;

(b) kukataa kutumia huduma muhimu;

(c) kuwafunga katika utaratibu;

(d) kuwabagua miongoni mwa wateja au wasambazaji; au

(e) vitendo vyengine vyovyote vinavyofanana na hivyo.

(5) Ni marufuku kwa mtu mwenye ukiritimba katika soko kujihusisha na mienendo ambayo ni:

(a) kwa njia moja au nyengine kupanga bei au masharti ya kuuza kwa mara nyengine;

(b) kuwaondoa wateja au washindani kutoka katika upatikanaji wa vyanzo vya usambazaji au kuwatoa katika upatikanaji wa njia za kufikia kwenye masoko;

(c) kuzuwia taratibu za upelekaji wa bidhaa au huduma katika maeneo mbalimbali ya kijografia;

(d) kutumia haki za mali bunifu kwa njia yoyote ile ambayo imevuka mipaka ya ulinzi wake wa kisheria; au

(e) vitendo vyengine vyovyote vinavyofanana na hivyo.

(6) Mtu anaekiuka masharti ya kifungu hiki ametenda kosa.

Miungano na ununuzi wa Mashirika.

49.-(1) Miungano au manunuzi yoyote ya shirika ambayo yatajenga au kuimarisha ukiritimba katika soko inayoharibu ushindani imekatazwa.

(2) Iwapo miungano ya mashirika itafanya au itaimarisha ukiritimba katika soko chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hichi, Tume itatathmini nguvu ya ushindani huo katika soko husika kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

(a) kiwango halisi cha upatikanaji wa ushindani katika soko;

(b) urahisi wa kuingia na kutoka katika soko, ikijumuisha vikwazo vya ushuru na kisheria;

(c) kiwango cha kuwekeza katika soko;

(d) kiwango cha nguvu za kukabiliana na soko;

(e) muungano ambao utapelekea kuongeza bei au faida;

(f) kiwango ambacho mbadala unavyopatikana katika soko;

(g) ufanisi katika soko ikiwa ni pamoja na ukuaji wa soko lenyewe, ubunifu, na utofautishaji wa bidhaa;

(h) ikiwa miungano hiyo itasababisha kuondolewa mshindani imara;

(i) uwepo wa kiwango cha ushirikiano wima ambao utasababisha uwiano wa kibiashara katika soko; na

(j) miungano inayoleta au inayoweza kuleta faida kwa Umma yanatarajiwa kuleta manufaa kwa umma katika moja au zaidi ya mambo yafuatayo:

(i) kwa kuchangia ufanisi kwa kiwango cha juu katika uzalishaji au usambazaji;

(ii) kwa kuchochea maendeleo kiutaalamu au kiuchumi;

(iii) kwa kuchangaia ufanisi kwa kiwango cha juu katika mgao wa rasilimali:

(iv) kwa kuhifadhi mazingira na miungano;

(v) kuzuiya, kukwaza au kuvuruga ushindani kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko kuleta manufaa; na

(vi) manufaa kwa umma yanayotokana na miungano hiyo yanazidi madhara yanayotokana na kuzuia kukwaza au kuvuruga ushindani.

(3) Baada ya kufanya utafiti wa miungano hiyo, Tume itaruhusu miungano hiyo kuendelea kutekeleza kazi zake au kuzuia kutekeleza kazi hizo ikiwa inaathiri ushindani katika soko.

(4) Waziri anaweza kufanya mapitio ya maamuzi yaliyotolewa na Tume kuhusu miungano hiyo ikiwa akiridhika kwamba:

(a) maamuzi yaliyotolewa yalitokana na taarifa zisizo sahihi;

(b) ithibati ilipatikana kwa njia ya uongo;

(c) kampuni hizo husika zilitengua wajibu au masharti yaliyofunganishwa katika maamuzi;

(5) Mtu anaekwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki ametenda kosa.

Taarifa, uchunguzi, kuzuia miungano ya makampuni, na ikiritimba katika soko.

50. Miungano, uchukuaji, ubia, au ununuzi wowote wenye lengo la kudhibiti, ikijumuisha na mfungamano wa wakurugenzi, ikiwa ya usawa, wima au kundi la miungano litambulishwe kwa Tume ikiwa:

(a) angalau moja katika mashirika hayo yawe yameanzishwa katika nchi; na

(b) mgao wa hisa katika soko nchini, au sehemu muhimu ya shirika hilo inayohusiana na bidhaa au huduma ambayo inaweza kupelekea uwepo wa nguvu za soko hasa katika viwanda ambavyo vina viwango vikubwa vya uwekezaji katika soko, pale ambapo kutakuwa na vikwazo vya kuingia au kuwepo kwa upungufu wa mbadala wa bidhaa zinazosambazwa na makampuni ambayo mienendo yake ipo katika uchunguzi.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YANAVYOHUSIANA NA MIENENDO YA UPOTOSHAJI NA UDANGANYIFU

Mienendo ya upotoshaji na udanganyifu

51. Ni marufuku kwa mfanyabiashara au muuzaji yoyote wa jumla au muuzaji wa rejareja kujihusisha na mienendo ya udanganyifu au upotoshaji au yenye muelekeo wa kuwapotosha au kuwadanganya watumiaji.

Udanganyifu au upotoshaji.

52.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kujihusisha na mienendo ifuatayo katika kufanya usambazaji wa bidhaa au huduma:

(a) kutoa maelezo ya uongo kuwa bidhaa ni ya kiwango, ubora, daraja, sifa, mtindo, au modeli fulani au ni yenye historia au matumizi fulani kabla ya iliyonayo;

(b) kutoa maelezo ya uongo kuwa huduma ina kiwango cha ubora au daraja fulani;

(c) kutoa maelezo ya uongo kuwa bidhaa ni mpya au ina miaka mahsusi;

(d) kutoa maelezo ya uongo kuwa mtu fulani amekubalia kupata bidhaa au huduma;

(e) kutoa maelezo ya uongo kuwa bidhaa au huduma zina udhamini, kibali, ufanisi, viambato, matumizi au manufaa zisizokuwa nazo;

(f) kutoa maelezo ya uongo kuwa ana udhamini kibali au ushirikiano ambao hana;

(g) kudanganya au kupotosha kuhusu bei ya bidhaa au huduma;

(h) kudanganya au kupotosha kuhusu upatikanaji wa huduma za kukarabati bidhaa au vipuri;

(i) kudanganya au kupotosha kuhusu uasili wa bidhaa;

(j) kudanganya au kupotosha kuhusu mahitaji ya bidhaa zozote zile; au

(k) kudanganya au kupotosha kuhusu uwepo, uondoaji au matokeo ya hali yoyote, waranti, dhamana kwa bidhaa, haki au fidia.

(2) Mtu anaekiuka masharti ya kifungu hiki ametenda kosa.

SEHEMU YA SITA
VITENDO VISIVYOKUBALIKA KATIKA BIASHARA

Matangazo yenye hadaa.

53.-(1) Ni marufuku kwa mtu kutangaza kuwa ana uwezo wa kufanya usambazaji wa bidhaa au kuuza bidhaa au huduma kwa bei mahsusi huku akijua kuwa hana uwezo wa kumpatia mteja au mtumiaji bidhaa au huduma hizo kwa bei hiyo.

(2) Mtu yeyote katika biashara ambaye ametangaza bei kwa ajili ya usambazaji wa bidhaa au huduma atalazimika kutoa bei hiyo kwa kipindi muwafaka kwa kutilia manani hali halisi ya soko analofanyia biashara na hali halisi ya tangazo lake.

(3) Ikiwa mtu aliyeainishwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki ameshindwa kutoa bidhaa au huduma kwa bei aliyoitangazia, anaweza:

(a) kumpa mtu mwengine kufanya usambazaji wa bidhaa au huduma za aina iliyotangazwa kwa Mtumiaji kwa muda muafaka, kwa kiwango muafaka , na kwa bei iliyotangaziwa, au;

(b) kusambaza haraka iwezakanavyo, au kumpa mtu mwengine kusambaza kwa mteja bidhaa au huduma zinanazolingana katika muda muafaka, kwa kiwango muafaka na kwa bei ya bidhaa au huduma zilizotangaziwa.

Kukubali malipo bila ya kukusudia au kutoweza kutekeleza usambazaji wa bidhaa au huduma.

54. Ni marufuku kwa mtu kupokea malipo au kitu chengine kwa ajili ya bidhaa au huduma ambapo wakati wa kupokea anajua kwamba:

(a) hana uwezo wa kusambaza bidhaa au huduma; au

(b) atasambaza bidhaa au huduma tofauti na bidhaa na huduma ambazo malipo yake ameyapokea; au

(c) kuna sababu za kuridhisha ambazo anazitambua kuwa zitamfanya ashindwe kusambaza bidhaa au huduma hizo ndani ya kipindi alichokiainisha, na kama kipindi hakikuainishwa, ndani ya muda muafaka.

Biashara isiyo kubalika.

55.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya biashara isiyo halali ikiwemo njia tafauti za udanganyifu , uwongo, au utaratibu ulio kinyume na maadili ili kujipatia au kujihusisha na biashara.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki biashara isiyo halali inajumuisha upotoshaji, matangazo ya uongo, kuwazuia watu kuuza, na matendo mengine ambayo yametamkwa bayana kuwa si halali kwa mujibu wa Sheria hii.

Viwango salama.

56. Ni marufuku kwa mtu yeyote kusambaza bidhaa yoyote ambayo:

(a) itapelekea kusababisha madhara ya afya au madhara ya kimwili kwa mtumiaji wakati imetumiwa kwa usahihi; au

(b) ambayo haiendani na viwango vya Mtumiaji ambavyo vimeelezwa chini ya sheria yoyote.

Bughudha na vitisho.

57. Ni marufuku kwa mtu kutumia nguvu au bughuza au vitisho kuhusiana na usambazaji au uwezekano wa usambazaji wa bidhaa au huduma kwa mtumiaji au malipo ya bidhaa au huduma kutoka kwa mtumiaji.

SEHEMU YA SABA
MASHARTI YANAYOHUSIANA NA KUMLINDA MTUMIAJI

Uuzaji wa bidhaa.

58. Mtu anaruhusiwa kusambaza au kuuza bidhaa zile tu ambazo zimethibitishwa kuwa na ubora na zinafaa kwa matumizi ya binadamu chini ya sheria zilizopo.

Kuoneshwa kwa bei.

59.(1) Muuzaji, mfanyabiashara, au muuzaji rejareja atatakiwa kubandika bei za bidhaa anazouza au huduma anayoitoa kwa watumiaji.

(2) Mtu anaekwenda kinyume na kifungu hiki,ametenda kosa na ikithibiti atatozwa faini ambayo sio chini ya Shilingi Millioni Moja na haitozidi Shilingi Millioni Tano au atatumikia kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita au vyote viwili.

Dhamana kwa bidhaa.

60.-(1) Muuzaji wa vifaa vya kielektroniki, vya umeme, au vifaa vya ujenzi atatakiwa kutoa hati ya dhamana kwa mtumiaji wakati wa mauzo.

(2) Muuzaji alieainishwa katika kifungu kidogo cha(1) cha kifungu hiki anatakiwa kukibadilisha, kukitengeneza, au kulipa gharama ya bei ya bidhaa alizoziuza ikiwa kama bidhaa hiyo zitakuwa na hitilafu zilizobainika ndani ya muda ulioanishwa katika dhamana.

(3) Muuzaji wa vipodozi, dawa, sabuni, na dawa za kusafishia, vifaa vya elektroniki na vya umeme, anatakiwa atoe maelekezo ya matumizi ya bidhaa hizo.

(4) Mtoa huduma anatakiwa kumhakikishia mtumiaji kwamba atampatia huduma nyengine ya ziada iwapo atapata athari yoyote au hasara kutokana na huduma zake na atarejesha gharama za bei iliyoainishwa au kumfidia ndani ya muda ulioainishwa.

(5) Masharti ya dhamana au huduma ya ziada kutoka kwa muuzaji au mtoa huduma kwa mtumiaji zitaelezwa bayana wakati wa mauziano.

Muundo wa bei.

61.-(1) Waziri ataandaa na kuchapisha katika Gazeti Rasmi la Serikali muundo wa bei kwa bidhaa zilizodhibitiwa kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Biashara na kanuni zake.

(2) Muundo wa bei utatayarishwa baada ya kuzingatia:

(a) kupanda na kushuka kwa bei ya soko la ndani;

(b) bei ya soko la Dunia;

(c) mabadiliko ya ubadilishaji wa thamani ya fedha; na

(d) sababu nyengine yoyote ambayo inahusisha upandaji na ushukaji wa bei katika soko.

(3) Muuzaji au msambazaji anaweza, wakati wowote ambapo bei ya soko la bidhaa zinazodhibitiwa zimebadilika, kumuomba Waziri kufanya mapitio ya muundo wa bei hizo.

(4) Muuzaji au msambazaji anatakiwa kuuza bidhaa zake katika bei ambayo haitozidi bei iliyopangwa katika muundo wa bei.

(5) Bila ya kuathiri sera za uchumi wa soko huria na biashara huria, Waziri anaweza kusimamia bei ya bidhaa yeyote kama kutatokea upandaji mkubwa wa bei katika soko na upandaji huo unaathiri watumiaji.

(6) Utaratibu wa uandaaji wa muundo wa bei kwa bidhaa zilizodhibitiwa, na udhibiti kwa bidhaa nyengine ambazo zina bei kubwa, utaelezwa kwenye kanuni.

Wajibu wa wazalishaji au Wakala wa Bidhaa.

62.-(1) Wazalishaji au mawakala wa bidhaa wanapaswa kuzingatia mambo yafuatayo wakati wanasambaza bidhaa kwa mtu mwengine:

(a) maelezo ya bidhaa yanayohusiana na maombi;

(b) bidhaa zinalingana na sampuli;

(c) sifa za bidhaa ziko sahihi;

(d) bidhaa zinakidhi vigezo vya msambazaji au mtumiaji;

(e) bidhaa ziwe na sifa za kuuzika.

(2) Mzalishaji au wakala ambae atashindwa kukidhi vigezo vilivyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki ametenda kosa na itakapothibitika atawajibika kulipa fidia kwa msambazaji au mtumiaji kutokana na hasara au uharibifu uliotokea wakati wa usambazaji.

Kuzuia bidhaa kusambazwa.

63.-(1) pale ambapo bidhaa itaonekana ina dosari, itasababisha madhara, ina hatari kwa watumiaji, haikidhi viwango au inasifa hatarishi, itatamkwa bayana kuwa haifai kwa matumizi ya binadamu.

(2) Waziri atatoa amri kwa msambazaji au mzalishaji kuondoa bidhaa sokoni kwa gharama za msambazaji au mzalishaji.

(3) Bidhaa yoyote iliyoondolewa sokoni itaangamizwa kwa mujibu wa taratibu zilizoelezwa chini ya kanuni.

Marufuku kwa bidhaa zisizosalama.

64.-(1) Ni marufuku kwa mtu yoyote kusambaza au kuuza bidhaa kwa mtumiaji ikiwa:

(a) ikiwa bidhaa hakidhi viwango vinavyotakiwa;

(b) bidhaa sio salama kwa matumizi ya binadamu;

(c) ikiwa uingizaji au usambazaji wa bidhaa hizo zimepigwa marufuku Zanzibar; au

(d) tarehe ya bidhaa hizo zimemalizika muda wa matumizi.

(2) Kwa utekelezaji mzuri wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, sheria zinazo simamia masuala ya viwango na usalama wa bidhaa zitatumika ipasavyo.

Marufuku kwa bidhaa bandia.

65.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kujihusisha na uagizaji, usambazaji au uuzaji wa bidhaa bandia katika soko.

(2) Mtu atakuwa amejihusisha na vitendo vya bidhaa bandia ikiwa;

(a) ameghushi alama yoyote ya biashara;

(b) kufanya udanganyifu kwa bidhaa kwa alama ya biashara au alama nyengine yoyote ambayo kwa karibu sana inafanana na alama hiyo ya biashara na kwa lengo la kutaka kudanganya;

(c) kutengeneza miundo, umbile, mashine, au zana nyengine kwa madhumuni ya kughushi, au kutumika katika kughushi alama ya biashara;

(d) kutoa maelezo yoyote ya uongo kwa bidhaa; au

(e) kubadilisha au kuwa katika milki yake muundo, umbile, mashine, au zana nyengine kwa madhumuni ya kughushi alama ya biashara.

(3) Mtu anaekwenda kinyume na msharti ya kifungu hiki ametenda kosa.

Kukamata bidhaa zisizosalama na bidhaa bandia.

66. Itakuwa ni wajibu wa Tume kukamata bidhaa yoyote itakayoonekana haiko salama au bandia.

Kuharibu bidhaa zisizosalama na bandia.

67.-(1) Bidhaa yoyote itakayobainika si salama na bandia itaharibiwa na Tume kwa kufuata utaratibu kama utakavyoelezwa kwenye kanuni.

(2) Tume itatathmini gharama za ukamataji au za kuharibu bidhaa hizo na gharama hizo zitatolewa na mzalishaji, muuzaji au msambazaji.

(3) Tume itatoa hati ya kuharibu baada ya kuharibu bidhaa zisizosalama au bandia.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI YA JUMLA

Maelekezo ya Waziri.

68. Waziri anaweza kutoa maelekezo kwa Tume kwa jumla au kwa kuainisha kwa lengo la kufanikisha shughuli zake na Tume itayatekeleza maelekezo hayo kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Utekelezaji wa amri na makubaliano ya utekelezaji.

69.-(1) Pale ambapo Tume itaridhika kwamba mtu ametenda au anaelekea kutenda kosa dhidi ya Sheria hii isipokuwa Sehemu ya Nne au ya Tano, inaweza kutoa amri ya utekelezaji chini ya kifungu hiki dhidi ya mtu huyo na mtu mwengine yeyote aliyehusika kwenye kosa.

(2) Mtu atakaeshindwa kutekeleza amri iliyotolewa dhidi yake, ametenda kosa.

(3) Amri ya utekelezaji inaweza kumtaka mtu kujiepusha na mienendo inayokwenda kinyume na Sheria au kuchukua hatua ya kutekeleza Sheria hii, na itaainisha muda wa utekelezaji wa amri hiyo na kipindi cha kutumika kwa amri hiyo husika.

(4) Tume inaweza kuweka amri ya muda wa mpito wa amri ya utekelezaji ikusubiri kutafakari shauri liliopo mbele yake ikiwa Tume itaona kwamba kuna uwezekano wa kuwepo hatari ya madhara makubwa kwa mtu kama vitisho au kosa kama hilo kutendwa au kuna sababu nyengine za msingi za kutoa amri hiyo.

(5) Bila ya kuwekea mipaka masharti ya ujumla ya kifungu kidogo cha (3)cha kifungu hiki , iwapo Tume imeridhika kwamba mtu ambaye kwenye kifungu hiki kidogo atatajwa kama "mpataji" amepata hisa au mali kwa kukiuka kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 49, Tume

inaweza kutoa amri wakati wowote ndani ya kipindi cha miaka mitatu baada ya upataji huo:

(a) kumtaka mpataji kutoa kiasi cha hisa au mali yote ndani ya muda ambao Tume itabaanisha kwenye amri husika, au

(b) kutamka kuwa upatikanaji huo ni batili pamoja na kumtaka mpataji kuhamisha baadhi au hisa zote au mali zote kurudisha kwa mtu ambae mpataji amepata hisa au vitu kutoka kwake kwa mujibu wa kifungu kidogo hiki ametajwa kama " mchuuzi" na kumtaka mchuuzi kumrejeshea mpataji baadhi au kiasi chote cha fedha alichopokea mchuuzi kuhusiana na upatikanaji, kama Tume itakavyobainisha kwenye amri.

(6) Bila kuweka mipaka ya ujumla ya masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, iwapo Tume itaridhika kwamba mtu ametenda kosa dhidi ya Sheria hii isipokuwa chini ya Sehemu ya Nne na ya Tano, Tume inaweza kuamuru mtu huyo atangaze, kwa namna na ndani ya muda ambao Tume itaona unafaa kwa taarifa hiyo kutangazwa kuhusiana na kosa.

(7) Amri ya utekelezaji itatolewa kwa maandishi ikianisha sababu za kutoa amri hiyo.

(8) Tume inaweza kuingia kwenye makubaliano kwa maandishi yaliyotajwa katika kifungu hiki kama “makubaliano ya utekelezaji”, ambapo mtu anaahidi kwa Tume kuepuka kutenda matendo yanayokwenda kinyume na Sheria hii kuanzia tarehe, na katika muda, ulioainishwa katika makubaliano ya utekelezaji au wa kutoa hisa au rasilimali na mambo mengine yaliyotajwa kwenye kifungu kidogo cha (3)cha kifungu hiki, kwa makubaliano na masharti kama ambavyo Tume itakavyoona inafaa.

(9) Amri ya utekelezaji itakuwa na nguvu kisheria sawa sawa na amri iliyotolewa na Mahakama kuu.

(10) Nakala ya amri ya utekelezaji au ya makubaliano ya utekelezaji yatawekwa kwenye Rejista la Umma, na kama ni amri ya utekelezaji, nakala itapelekwa kwa mtu ambae amri imetolewa dhidi yake.

(11) Bila ya kuathiri sheria yoyote, nakala ya Amri ya utekelezaji au ya makubaliano yaliyothibitishwa na Tume yatakuwa ni ushahidi wa mwisho kwenye Mahakama yoyote itakayotoa amri na sababu za kufikia amri hiyo au kufikia utekelezaji wa makubaliano hayo.

(12) Tume haitakuwa na mamlaka kisheria kutoa amri ya utekelezaji au kuingia katika makubaliano ya utekelezaji yanayoelekea kuvunja masharti au haki iliyoelezwa kwenye sehemu ya Nne na ya Tano au wajibu wa mzalishaji kwenye sehemu ya Saba.

Kukinzana na sheria nyengine.

70.-(1)kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki tu, Sheria hii itatumika kwa watu wote walio kwenye sekta zote za uchumi na haitafutwa, kuondolewa au kurekebishwa:

(a) na sheria nyingine yoyote isipokuwa tu pale ambapo sheria itapitishwa baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii inayotengua au kurekebisha Sheria hii; au

(b) na sheria ndogo iwe au isiwe hiyo sheria ndogo inakusudia kutengua au kurekebisha Sheria hii.

(2) Mtu hatakuwa amevunja masharti ya Sheria hii kwa sababu tu ya kujihusisha na mwenendo, isipokuwa katika masharti yaliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki:

(a) kumtaka mtu kujiingiza kwenye mwenendo au mwenendo unaofanana na huo; au

(b) kumuidhinisha au kumthibitisha mtu anayejihusisha au anayejizuwia kujihusisha kwenye mwenendo wa aina hiyo.

(3) Sheria zilizorejewa kwenye kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki ni ya ZURA, sheria ya ZMA, sheria ya ZFDA, sheria ya Biashara, sheria ya Viwango, na sheria za sekta, sheria za kulinda mazingira na sheria ndogo au chombo chochote chini ya sheria ambazo zimetajwa.

(4) Pale ambapo Tume itakuwa na maoni kwamba mwenendo wowote unahitajika uloidhinishwa au umekubaliwa na Mamlaka yaUdhibiti iliyorejewakatikakifungukidogo cha (3), itakuwa ni uvunjajiwa sharia hii kama kifungu kidogo cha (1), hakitumiki kwenye mwenendoTume itaripoti jambohilo kwa Waziri.

(5) Pale ambapo Waziri atapokea ripoti kutoka kwa Tume chini ya kifungukidogo cha (4), anaweza kuelekeza Mamalaka ya Udhibiti husika kuchukua hatua za lazima kuhakikisha kwamba mwenendo uliyoelezwa na Tume hauhitajiki, hauidhinishwi na Mamlaka ya Udhibiti.

Rufaa.

71. Mtu aliyeathiriwa na maamuzi yaliyofanywa na Tume chini ya Sheria hii na maamuzi ya mamlaka nyengine za udhibiti anaweza kukata rufaa kwa Baraza.

Makosa ya ujumla na adhabu.

72.-(1) Mtu anayekwenda kinyume na masharti ya Sheria hii au anashindwa kutekeleza amri za Tume, za Waziri,au za Baraza ametenda kosa chini ya Sheria hii, Endapo hakuna adhabu maaalumu iliyoweka, atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja na isiyozidi Shilingi Milioni Tano au Kifungo cha mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

(2) Ikiwa Tume imeridhika kwamba thamani ya fedha inaweza ikawekwa kufidia hasara iliyopatikana kwa mtu kwa matokeo ya kosa dhidi

ya Sheria hii, mtu aliyetiwa hatiani atakuwa na wajibu, kwa kuongezea adhabu ambayo inaweza kutolewa faini, kulipa faini mara mbili ya thamani ya fedha hizo, ambazo Mkurugenzi Mkuu ataagiza zilipwe kwa mtu aliyepata hasara hiyo.

(3) Mtu anayekwenda kinyume na kifungu cha 43, 45 na 61 hawatawajibika kutozwa faini chini ya kifungu hiki lakini anaweza kuwajibika kukubali Amri za utekelezaji na Amri za fidia kwa anayepata hasara au madhara.

Adhabu ya papo kwa papo.

73. Tume inaweza kutoa adhabu ya papo kwa papo kwa kosa lolote lililofanywa na mtu chini ya Sheria hii au kanuni zake kwa kumtaka alipe faini itakayowekwa kwa kosa hilo, kwa masharti kwamba mtu huyo:

(a) anakubali kwa maandishi kuwa ametenda kosa hilo na atakua na tahadhari kubwa kwamba hatorejea tena kosa hilo; na

(b) analipa fedha nyengine anazowajibika kulipa chini ya Sheria hii au kanuni zake.

Kanuni.

74. Waziri ataandaa kanuni zifuatazo kwa kwa ajili utekelezaji bora wa Sheria hii.

(a) kumlinda mtumiaji;

(b) ushindani halali;

(c) utaratibu wa fomu zitakazotumika chini ya Sheria hii;

(d) taratibu zinazohusiana na jumuia za watumiaji;

(e) taratibu za ukamataji na za kuharibu bidhaa;

(f) taratibu za utarayarishaji za muundo wa bei;

(g) taratibu za kuondoa bidhaa sokoni;

(h) taratibu za ukaguzi;

(i) taratibu zinazohusiana na udhibiti wa bidhaa bandia; na

(j) mambo mengine yatakayoonekana muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

75.-(1) Sheria ya Zanzibar ya kusimamia mwenendo wa Biashara na kumlinda Mtumiaji Nam. 2 ya mwaka 1995, inafutwa.

(2) Bila ya kujali Sheria iliyofutwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kanuni zote, miongozo iliotungwa na jambo lolote lililofanywa chini ya Sheria zilizofutwa kabla ya kuanza kutumika Sheria hii itachukuliwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii hadi wakati ambapo sheria ndogo inayokusudiwa imefutwa na kutungwa nyengine.

MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Mswada huu ni kuimarisha ustawi wa watu wa Zanzibar kwa ujumla kwa kuboresha na kulinda ushindani imara katika soko na kuzuia mwenendo ulio potofu na danganyifu katika soko kwa Zanzibar nzima ili:

(a) kuongeza ufanisi katika uzalishaji, usambazaji na ugavi wa bidhaa na huduma;

(b) kukuza ubunifu;

(c) kufikia kiwango cha juu cha ufanisi katika utumiaji wa rasilimali; na

(d) kuwalinda walaji.

Mswada huu unakusudia kuanzisha Tume ya Ushindani na Baraza la Ushindani Halali ambalo lina jukumu ya kusimamia, kudhibiti na kuzuia matendo yoyote yanayoathiri ushindani na uendeshaji wa biashara halali Zanzibar, na kusikiliza na kuamua rufaa zinazotokana na amri na maamuzi na Tume ya Ushindani Halali wa Biashara na Mamlaka nyengine za usimamizi.

Kwahiyo, Mswada unalenga kuipa uwezo Tume katika kukuza na kulinda ushindani imara wa kibiashara , kuwalinda watumiaji dhidi ya mwenendo mbaya na potoshi katika soko.

Mswada unapendekeza kuanzisha uongozi imara ambao utakuwa chini ya Mkurugenzi Mkuu ambae atakuwa mtendaji Mkuu wa Tume. Kwa madhumuni hayo, Mkurugenzi Mkuu atakuwa na wajibu wa kuongoza chini ya Tume kwa kutumia ujuzi na utaalamu alionao ili kutoa huduma nzuri kwa wateja waliokusudiwa. kwa kuongezea, Mkurugenzi Mkuu atakuwa ni Mkuu wa Sekretarieti ya Tume ambaye ataratibu na kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Tume.

Juu ya yote, Tume itafanya majukumu yake yaliyoainishwa kisheria chini ya maelekezo kutoka Tume.

Mswada unaweka misingi ya utawala kwa Tume ambayo itasaidia kuhakikisha usimamizi mzuri wa fedha katika kupanga bajeti, kuhifadhi baadhi ya asilimia ya fedha zinazokusanywa, kukusanya mapato, kuwasilisha ripoti ya fedha kwa Waziri na masuala mengine yoyote yanayohusiana na hayo kwa mujibu wa miamala ya fedha iliyokubalika kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na kanuni zake.

Mswada huu umegawika katika Sehemu Nane kama ifuatavyo:

SEHEMU YA KWANZA inahusu masharti ya utangulizi ambapo inajumuisha Jina fupi, Ufafanuzi wa baadhi ya maneno, pamoja na Matumizi ya Sheria hii.

SEHEMU YA PILI inahusu uanzishwaji na uendeshaji wa Tume ambayo ndani yake unaelezea, muhuri wake, nembo yake, kazi zake, uwezo wa Tume, sehemu hii pia inaelezea uongozi na uendeshaji wa Tume ambao unajumuisha

(a) Wajumbe wa Tume;

(b) Sekretarieti na waajiriwa wa Tume, ambao itajumuisha uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu, kazi za sekretarieti, uanzishwaji wa vitengo vya Tume , pamoja na uanzishwaji wa Jumuiya za watumiaji;

(c) Vikao vya Tume, ukomo wa wajumbe , kuanzisha lalamiko Usiri wa Tume , Mgongano wa kimaslahi na masuala yanayohusiana na masharti ya fedha yanayojumuisha fedha za Tume, utaratibu wa uandaaji wa bajeti na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

SEHEMU YA TATU inahusu uanzishwaji na uendeshaji wa Baraza la Ushindani halali ambayo inajumuisha:

(a) Muundo wa Baraza ambao unajumuisha Mwenyekiti na wajumbe wengine, kazi na uwezo wa Baraza.

(b) Inahusu Mrajis wa Baraza, kanuni za maadili, muhuri wa Baraza, maamuzi na maagizo ya Baraza, pingamizi kwa Baraza, kanuni za Baraza na masharti ya fedha yanayojumuisha fedha za Baraza na taratibu za uandaaji wa bajeti.

SEHEMU YA NNE inaelezea masuala yanayohusu mienendo ya biashara inayokatazwa, ambayo inajumuisha Mienendo ya biashara isiyo ya ushindani, mikataba ya biashara isiyo ya ushindani, Kuzuia na kukataza kuzambaza bidhaa, Matumizi mabaya ya nguvu za soko, Miungano na ununuzi wa mashirika, Taarifa, Uchunguzi , uzuwiaji wa miungano ya mashirika na ukiritimba katika soko.

SEHEMU YA TANO inatoa masharti yanayohusiana na Mienendo ya upotoshaji na udanganyifu inayojumuisha Udanganyifu au upotoshaji.

SEHEMU YA SITA inaelezea masuala yanayohusiana na vitendo visivyokubalika katika biashara ambavyo inajumuisha Matangazo yenye hadaa, Biashara isiyo halali, Viwango salama, Bughuza na vitisho.

SEHEMU YA SABA inahusu masharti yanayohusiana na kumlinda mtumiaji ambayo inajumuisha Uuzaji wa bidhaa, Kuoneshwa kwa bei, Dhamana kwa bidhaa, Muundo wa bei, Wajibu wa Mzalishaji au wakala wa bidhaa, Kuzui bidhaa kusambazwa, kuzuia ,kukamata na kuharibu bidhaa zisizosalama na bandia.

SEHEMU YA NANE inahusu masharti mengineyo ambayo yanajumuisha Maelekezo ya Waziri, Utekelezaji wa amri na makubaliano, Kukinzana na sheria nyengine, Makosa na Adhabu kwa wanaotenda uovu au mtu yoyote anaefanya au anaeacha kufanya lolote kinyume na masharti ya sheria hii atalazimika kulipa faini kwa namna ya kosa alilofanya. Vilevile sehemu hii inatoa mamlaka kwa Waziri kuandaa kanuni na Kufutwa na kubakiza.

MHE. BALOZI. AMINA SALUM ALI
WAZIRI WA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO
ZANZIBAR

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI - ZANZIBAR 2017